



Huyu ni Natabo.

Ana ndugu sita wa  
kiume.




Wazazi wake  
walimpatia chungu  
kidogo.

Alikipenda sana.




Siku moja, ndugu zake walikivunja chungu hicho.



Natabo hakukiona chungu chake.

Alilia kwa muda mrefu.




Natabo alitoroka  
nyumbani.

Alipanda mti mrefu.



Wazazi wake  
walimsihi,  
“Tafadhali, shuka  
chini.”



Ndugu zake waliimba, "Tafadhali, shuka chini."



Natabo aliufanyia  
mzaha wimbo wao.



Naye rafiki ya Natabo akaimba, "Tafadhali, shuka chini."



Rafiki yake aliimba  
mpaka Natabo  
akashuka chini.



Marafiki hao  
walienda nyumbani  
pamoja.



Walisherehekea.

Natabo alipata chungu kipya!